GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXII Nam. 6489 **17 Septemba, 2013** **Bei Shs. 3,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara Sura 134 na mambo yanayohusiana na hayo..... 357

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya kurekebisha Amri ya Barabara Sura 134.

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 9 Oktoba, 2013 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR (Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
17 Septemba, 2013 ***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.***

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa
SHERIA YA AMRI YA BARABARA (MAREKEBISHO) 2013

SHERIA YA KUREKEBISHA AMRI YA BARABARA SURA 134

IMEPITISHWA na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.

1.(1) Sheria hii inaweza kuitwa kama Amri ya Barabara (Marekebisho) ya 2013 na itaanza kutumika mara tu Rais atakapoisaini.

(2) Sheria hii itasomwa kwa pamoja na Amri ya Barabara Sura 134 amabayo katika sheria hii itarejewa kama sheria mama.

SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO YA VIFUNGU MBALI MBALI

Marekebisho ya kifungu cha 2.

2. Kifungu 2 cha sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo.

(i) kwa kulitafsiri upya neno "Mnyama" kama ifuatavyo:

"Mnyama" maana yake ni mnyama yeyote wa kufugwa ikijumuisha farasi, punda, mbuzi, kondoo, ng'ombe na wengineo.

(ii) katika tafsiri ya neno "mmiliki" neno "koloni" linafutwa na badala yake kuandikwa neno "Zanzibar" marekebisho hayo yatahusika popote penye neno "koloni" katika sheria mama.

(iii) kwa kuondoa na kubadilisha tafsiri ya neno "barabara za umma" kama ifuatavyo:

"Barabara za umma" maana ni barabara yoyote iliyotajwa katika jaduweli 1 ya Sheria hii na barabara yoyote ambayo inaweza kupewa na kupewa tena daraja na Waziri chini ya kifungu 3 cha Sheria hii kuwa ni barabara ya umma na inajumuisha kila barabara ambayo umma una haki ya kupita na itajumuisha njia zilizoko pande zote za barabara, mifereji yote, mitaro yote, kuta za mitaro, vivuko na madaraja zinazofungamana nazo, na ardhi yote ambayo si mali binafsi iliyopo katika eneo la hifadhi ya barabara husika.

(iv) kwa kuongeza neno Idara litakalorejewa na neno "mamlaka ya barabara".

(v) kwa kurekebisha tafsiri ya neno "vyombo" kwa kuongeza maneno 'ina maana ya vyombo vya usafiri barabarani vya aina yoyote ile'

(vi) kwa kuongeza marejeo kuhusiana na tafsiri za maneno yafuatayo.

"Jengo" maana yake ni ujenzi uliofanyika ukiwa na au bila ya kuwa na paa au ukuta, likijumuisha msingi, nyumba, viwanda, vibanda, na chochote cha maumbile kama hayo.

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya barabara.

"Machimbo" maana yake pahala ambapo kwa kawaida ni tundu au shimo ardhini ambamo hutolewa mawe, mchanga, udongo fusi au nyezo nyengine inayoweza kuhitajika kwa madhumuni ya kufungua, kutengeneza au kukarabati barabara zozote za umma.

"Barabara ya akiba" maana yake ni eneo la ardhi lililotajwa na kutangazwa na Waziri chini ya kifungu 8 cha Sheria hii iliyopo kila upande wa baarabara iliyopimwa kutoka katikati ya barabara kama hiyo.

"Barabara" maana yake ni eneo la wazi kwa au linalotumiwa na umma na linaendelezwa kwa ajili ya, au hutumika zaidi kwa, kuendeshea vyombo vya moto, na inajumuisha njia za kupitishia vigari vya punda, mikokoteni, njia za waendao kwa miguu au baiskeli, ikiwa zimewekewa lami au la, na nyengine kama hizo.

"Shilingi" maana yake ni shilingi ya Tanzania.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

3. Kifungu 3 cha sheria mama hapa kinarekebishwa kwa kufuta sharti lilowekwa kwa kifungu hicho.

Kufuta kifungu cha 4.

4. Kifungu 4 cha sheria mama kinafutwa.

Kufuta kifungu cha 5.

5. Kifungu 5 cha sheria mama kinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 6.

6. Kifungu 6 cha sheria mama kinarekebishwa kwa:

(i) kuondoa neno "Balozi Mkaazi wa Uingereza" na badala yake kuweka neno "Waziri"

(ii) kuondoa maelezo ya pembeni na badala yake kuandika yanayosomeka "Waziri anaweza kutangaza barabara za umma"

Marekebisho ya kifungu cha 7.

7. Kifungu 7 cha sheria mama kinarekebishwa kwa:

(i) kufuta maneno " kutokana na maombi ya mamlaka ya barabara, Balozi Mkaazi wa Uingereza" na badala yake kuandika neno "Waziri"

(ii) kufuta maneno " Balozi Mkaazi wa Uingereza" yaliyojitokeza baada ya maneno "Mamlaka ya barabara" na badala yake

kuandika neno "Waziri"; marekebisho haya yatahusu kila pahala ambapo maneno " Balozi Mkaazi wa Uingereza" yatajitokeza.

Marekebisho ya kifungu cha 8.

8. Kifungu 8 cha sheria mama kinarekebishwa kwa:

(i) kufuta maneno "Mgawanyo wa barabara za umma" yaliyopo katika maelezo ya pembeni na badala yake kuandika maneno "Waziri anaweza kuzigawa na kuzigawa tena barabara za umma"

(ii) kufuta maneno "Balozi Mkaazi wa Uingereza kwa kutoa notisi katika Gazeti rasmi la Serikali" na badala yake kuandika maneno "Waziri anaweza, kwa notisi iliyochapishwa katika Gazeti rasmi la Serikali".

Kuongeza kifungu kipya cha 8A.

9. Sheria mama hapa inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 8A kama ifuatavyo:

"Aina za barabara

8A. Kwa madhumuni ya Sheria hii mtandao wa barabara unagawiwa daraja tofauti kama ifuatavyo:-

(a) Barabara Kuu: Barabara ambazo kimsingi huunganisha mikoa miwili au zaidi.

(b) Barabara za Vijijini: Ni barabara zinazounganisha kijiji na kijiji kama inavyoonekana katika jaduweli.

(c) Barabara za Mjini: Ni barabara zinazounganisha Barabara Kuu na barabara nyengine ndani ya maeneo ya mji.

(d) Barabara za Kulishiza: Ni barabara ndogo vijijini ndani ya wilaya moja na mara nyingi huanzia kutoka barabara za Vijijini au barabara kuu kama ilivyooneshwa katika jaduweli.

(e) Barabara nyenginezo: Barabara nyengine zinajumuisha barabara zisizotajwa katika (a), (b), (c) na (d) ya kifungu hiki".

Kufutwa kwa kifungu cha 9.

10. Sheria mama inarekebishwa kwa kukifuta kifungu 9.

Marekebisho ya kifungu cha 10.

11. Kifungu 10 cha sheria mama kinarekebishwa kwa -

(i) kufuta maneno 'na iliyotengwa bila zabuni au malipo kwa njia ya fidia na kuanzia hapo itakuwa katika kabidhi ya Serikali bila uhaulishaji rasmi wowote juu yake' na badala yake kuandikwa maneno 'kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi Namba 12 ya 1992 pamoja na marekebisho yake;

(ii) kufuta maelezo ya pembeni na badala yake kuandika maneno "kupata ardhi kwa ajili ya barabara ya umma"

12. Kifungu 11 cha sheria mama kinarekebishwa kwa:- Marekebisho ya kifungu cha 11.

(i) kuondoa maneno "kama atakavyoona ni mantiki" na badala yake kuandika maneno "kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi Namba 12 ya 1992 kama ilivyorekebishwa kutoka wakati mmoja hadi mwengine pamoja na sheria nyengine yoyote inayotumika,

.

(ii) kufuta kijifungu (2) cha kifungu hiki.

13. Sheria mama inarekebishwa kwa kuingiza kifungu kipya 11A kama ifuatavyo: Kuongeza kifungu kipya cha 11A.

11A Waziri atasababisha mpango au ukaguzi kutayarishwe kuhusiana na barabara zote za umma zilizotangazwa chini ya sheria hii na katika nyakati tafauti atasababisha kupitishwa kwengine au mabadiliko yoyote yaliyofanywa katika barabara za umma zilizopo kuongezwa kwenye mpango au ukaguzi.

14. Kifungu 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno “iliyopelekwa kwa usuluhishi kwa mujibu wa kifungu cha 19” na kuweka badala yake maneno “iliyosuluhishwa kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria hii”. Marekebisho ya kifungu cha 15.

15. Kifungu 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kizima na kuweka badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo:- Marekebisho ya kifungu cha 19.

19.(1) Mtu ambae atakuwa hakuridhika na maamuzi ya Idara ya malipo au ya kiwango cha fidia yanayotokana na tendo lolote au jambo lolote lililofunywa na Idara kwa mujibu wa uwezo wake chini ya kifungu cha 13, atalazimika kupeleka ombi la maandishi kwa utaratibu uliowekwa na Sheria ya Fidia.

(2) Endapo itatokezea kutowepo kwa Sheria ya Fidia mtu huyo atalazimika kufungua shauri Mahakamani.

16. Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta maneno ya kifungu 20 na badala yake kuandika mengine kama yafuatavyo: Kufuta kifugu 20 na kukiandika upya.

20. Mtu yoyote anaepinga, anaeizuia, anaekwamisha, anaesumbua au kusasababisha kuzuiwa afisa aliyeidhinishwa na mamlaka katika kutekeleza majukumu yake, au kufanya kitendo chochote kilichoruhusiwa au alichotakiwa kufanya na sheria hii, atakuwa ametenda kosa na ikithibitika anatakiwa alipe faini isiyopungua laki tano na isiyozidi milioni moja au kifungo kisichozidi kipindi cha miezi mitatu.

17. Kifungu 21 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno 'Shilingi sabini na tano' yanayotokeza baada ya maneno 'isio pindukia' na badala yake kuandika maneno 'adhabu isiyopungua Shilingi Laki tano na isiyozidi Shilingi milioni moja na laki tano, na maneno 'wiki mbili' yatafutwa na badala yake kuandikwa 'miezi mitatu'. Marekebisho ya kifungu cha 21.

Kuongeza kifungu kipya cha 23A.

18. Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya kitachosomeka kama ifuatavyo:

"hifadhi ya barabara

23A.(1) Kutokana na maombi ya mamlaka ya barabara Waziri anaweza kuweka masafa fulani kutoka katikati ya barabara maalum kuwa ni hifadhi ya barabara hiyo.

(2) Ispokuwa pale ambapo mali binafsi imehifadhiwa kwa matumizi ya Idara masafa ya hifadhi ya barabara kutoka katikati ya barabara kwa kila aina ya barabara na pande zote mbili za barabara yatakuwa:

(1) Mita 15 kwa Barabara Kuu.

(2) Mita 12 kwa barabara zinazoungana na Barabara Kuu.

(3) Mita 10 kwa Barabara za Wilaya.

(4) Kwa barabara nyengine ni kama itakavyowekwa na Idara".

Marekebisho ya kifungu cha 24.

19.(1) Kifungu 24 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(i) kwa kufuta maneno 'futi ishirini na tano kutoka katikati ya barabara ya umma' na badala yake kuandika maneno 'akiba ya barabara';

(ii) kwa kuongeza kifungu kidogo (2) kinachosomeka kama ifuatavyo:

(2) Mtu yeyote au taasisi atakaekwenda kinyume na kijifungu (1) cha kifungu hiki atakuwa na hatia ya kutenda kosa na ikithibitika atastahili adhabu ya faini ya shilling mia tano elfuna sio zaidi ya shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote mbili pamoja na kuondosha mti au nyumba husika.

Marekebisho ya kifungu cha 25.

20. Kifungu 25 cha Sheria mama kinarekebishwa sehemu ya adhabu kwa kuongeza maneno 'sio chini ya shilingi milioni moja' na kufuta maneno 'sio zaidi ya shilingi mia nne hamsini elfu' baada ya neno 'adhabu' na badala yake kuandika maneno 'na sio zaidi ya shilingi milioni tatu', na miezi mitatu itabadilishwa kuwa miezi kumi na mbili.

Marakebisho ya kifungu cha 26.

21. Kifungu 26 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa -

(a) kufuta neno 'kujeruhi' lililopo kabla ya neno 'umma' kwenye maelezo ya pembeni na kuandika neno 'kuhasiri' badala yake;

(b) kufuta maneno 'isiyozidi shilingi mia nne hamsini elfu' baada ya neno 'adhabu' na badala yake kuandika maneno 'sio chini ya shilingi milioni moja na mia tano elfu na sio zaidi ya shilingi milioni tatu' na kwenye adhabu ya kifungo badala ya 'miezi mitatu' itakuwa 'miezi saba'.

Marekebisho ya kifungu cha 27.

22. Kifungu 27 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:-

(a) kufuta neno 'mpya' lililopo kabla ya neno 'umma' na pia kufuta neno 'kufanya' lililopo baada ya neno 'kabla' na badala yake kuandika neno 'kujenga' kwenye maelezo ya pembeni;

(b) kufuta maneno 'isiyozidi shilingi mia nne hamsini elfu' baada ya neno 'adhabu' na badala yake kuandika maneno 'sio chini ya shilingi milioni moja na sio zaidi ya shilingi milioni tatu' na maneno 'mieazi mitatu' badala yake yatakuwa 'miezi kumi na mbili au vyote pamoja'

Marekebisho ya kifungu cha 30.

23. Kifungu 30 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(i) kufuta maneno 'kuwaachia wanyama' yaliopo kabla ya maneno 'kwenye barabara ya umma' na badala yake kuandika neno 'kuzuia' kwenye maelezo ya pembeni.

(ii) kufuta maneno 'sio zaidi ya shilingi nia nne na hamsini' baada ya neno 'adhabu' na badala yake kuandika maneno 'sio chini ya shilingi mia tano elfu na sio zaidi ya shiling milioni moja';

(iii) kufuta maneno 'miezi mitatu' baada ya maneno 'sio zaidi' na badala yake kuandika maneno 'miezi sita pamoja na gharama za kuondosha kizuizi kama hicho'

(iv) kwenye kivuo chake, kufuta maneno 'sio zaidi ya shilingi mia nne na hamsini elfu' yaliopo baada ya neno 'adhabu' na badala yake kuandika maneno 'sio chini ya shilingi mia mbili elfu na sio zaidi ya shilingi mia tano elfu'.

Marakebisho ya kifungu cha 32.

24. Kifungu 32 cha Sheria mama kinarekebishw kama ifuatavyo:

(i) kenye kifungu kidogo (1), kwa kufuta maneno 'Balozi Mkaazi wa Kingerea anaweza kutunga kanuni' na badala yake kuandika maneno 'Waziri anaweza kuandaa taratibu kama itakavyolazimu kwa madhumuni ya kuviwezesha kutumika vifungu vya Sheria hii;

(ii) kwenye kifungu kidogo (2), kwa kufuta neno 'kanuni' na badala yake kuandika neno 'taratibul', na kufuta maneno 'shilingi mia nne na hamsini' na badala yake kuandika maneno 'shilingi milioni moja'.

Kuongeza kifungu kipya cha 30A.

25. Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 30A kama ifuatavyo:

"Kuhifadhi Magingira

30A. Mamlaka ya barabara iliyokabidhiwa uendelezaji, uongozi na utengenezaji wa barabara za umma chini ya dhmana yake, itafuata miongozo, taratibu au sheria zilizowekwa kuhusiana na uhifadhi wa mazingira na utupaji wa taka".

Kuongeza kifungu kipya cha 33.

26. Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 33 kama ifuatavyo:

Kuongeza kifungu kipy cha 34.

27. Sheria Mama inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 34 kama ifuatavyo:

34. Bila ya kujali masharti ya Sheria nyengine yoyote, kauli au maamuzi yanayohusiana na usimamizi wa barabara, Idara itakuwa na uwezo, majukumu, kazi na dhamana iliyopewa na Sheria hii na endapo patatokea mgongano au mwingiliano baina ya Sheria yoyote, kauli au maamuzi yanayohusiana na kazi na majukumu ya Idara, masharti ya Sheria hii ndio yatatumika.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni na sababu ya Mswaada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya vifungu mbali mbali vya Sheria ya Barabara sura 134.

Idara ya barabarani inashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kuondokana na kuwa vifungu vingi vya Sheria ya barabara sura 134 vimepitwa na wakati na haviendani na hali ya sasa ya mabadiliko na ufanyaji kazi.

Kwa misingi hiyo, Wizara imeamua kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha baadhi ya vifungu vya Sheria hiyo ili kuiwezesha Idara kutimiza wajibu wake ipasavyo.

Mswaada huu kimsingi umegawika sehemu kuu mbili:-

Sehemu ya kwanza: Inazungumzia utangulizi.

Sehemu ya pili: Kwa jumla ya vifungu 27, ambapo kila kifungu kimependekeza marekebisho maalum ya vifungu vya Sheria ya barabara sura 134.

Kifungu cha 2: Kinapendekeza kufanyiwa marekebisho kwenye ufafanuzi kuwa baadhi ya maneno yanafutwa na kutolewa ufafanuzi upya.

Kifungu cha 3: Kinapendekeza kufuta proviso ya kifungu hicho.

Kifungu cha 4: Kinapendekeza kufuta kwa kifungu cha 4 na 5.

Kifungu cha 6na 7: Kinapendekeza kufuta maneno *"British Resident"* na kuweka baada ya neno "Waziri".

Vifungu vingine ambavyo vimependekezwa kufanywa marekebisho ni kama vifuatavyo:-

Kifungu cha 9: Kinapendekeza kufanya mabadiliko kwa kuongeza kifungu kipya cha 8A mara tu baada ya kifungu cha 8. Kifungu 8A kinaweka masharti ya aina za barabara.

Kifungu cha 13: Kinapendekeza kuongeza kifungu cha 11A mara tu baada ya kifungu cha 11.

Kifungu cha 15: Kinapendekeza kuweka utaratibu wa kufuatwa na mtu ambaye atakuwa hakuridhika na maamuzi yaliyotolewa dhidi yake.

Kifungu cha 18: Kinapendekeza kuweka kifungu kipya cha 23A ambacho kitaweka masharti ya maeneo ya hakiba ya barabara.

Kifungu cha 24: Kinapendekeza kuongeza kifungu cha 30A ambacho kinaweka masharti ya hifadhi ya Mazingira.

ZANZIBAR
17 Septemba, 2013

(RASHID SEIF SULEIMAN)
Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano